

Toleo: 1442/02 H

Jumatano, 06 Safar 1442 H

23/09/2020 M

Taarifa kwa Vyombo vyatuhusu

Ni Khilafah Pekee kwa Mfumo wa Utume Ndio Itakayositisha Ubabe wa Marekani na Kuikomboa Filastin

Utarawala wa Marekani umeitaka Kenya kuunga mkono maslahi ya kisiasa na kibashara ya taifa la 'Israel' la sivo iachane kabisa na mkataba wa kibashara huria (Free Trade Deal- FTA) iliosaini na taifa hilo kubwa la kiuchumi duniani. Washington umeitaka Kenya kuwa ili kuimarishe ushirikiano wa Kibashara itapaswa kutounga mkono vitendo vitakavyohujumu biashara katika Marekani na utarawala wa Kizayuni.

Matamshi haya ya Amerika kwa Kenya, hayaoneshi tu ubeberu na ubabe wa sera yake ya kigeni bali pia yanaashiria kuwa Marekani ndio inayounga mkono na kudhamini jinai kubwa dhidi ya Waislamu wa ardhi tukufu ya Filastin. Siasa ya nje ya Marekani imejikita katika kuyaingilia mataifa mengine duniani na kuendesha sera zake za kigeni. Kiuhakika kwa kuwa Kenya kama nchi yoyote ile barani Afrika bado ingali chini ya minyororo ya ukoloni mambo leo hivyo katu haitoweza kuhimili kwa nguvu shnikizo la siasa la Kimarekani dhidi yake. Na ni kwa muktadha huu, Kenya tayari imekuwa ikitambua uwepo wa umbo la Kiyahudi na kuunga mkono suluhisho la serikali mbili kwa Filastin na utarawala wa Kizayuni.

Ombi hili la kibabe linakuja siku chache tu baada ya mataifa ya Muungano wa falme za Kiarabu na Bahrain kutia saini na utarawala haramu wa Kiyahudi kwenye makubaliano ya khyana kubwa dhidi ya ardhi ya Filastin huko Washington. Ni wazi kwamba Marekani ndio inayoendesha mipango na sera zote za kusimamisha serikali ya kujitawala ya Palestina pamoja na kuifanya Al-Quds ni miliki ya watu wa mataifa yote kuigawanya baina ya Waislamu na Mayahudi. Amerika aidha, ni mwekaji wa mikakati yote juu ya kadhia ya Filastin na kwamba anafanya kila awezavyo ili Waislamu wapate kudhurika.

Tunasema umbo la Kiyahudi liko ndani ya nchi ya Kiislamu na bila ya ardhi hii umbo hili haliwezi kuweko au pia kuendelea na ukaaji wake wa kimabavu. Utarawala huu haramu umenyakua ardhi ya Filastin ambayo ndani yake kuna Msikiti Mtukufu wa Al-Aqsa; kibla cha kwanza kwa Waislamu na Msikiti mtukufu wa tatu. Hivyo basi, kujenga mahusiano yote ya kimataifa au maslahi ya kibashara na kuhalalisha uwepo wake ni kitendo cha haramu kinachokataliwa na Dini yetu.

Kadhia ya Filastin ni kadhia ya Kiislamu hivyo tunakataa katakata suluhisho lolote lile la kimaghribi lisilokuwa la Kiiislamu. Kwa kutilia maanani uhalsia huu, ndio tunafanya kazi pasina kuchoka ya kurudisha sheria za Kiislamu katika mataifa ya Kiislamu chini ya utarawala muongofu wa Khilafah kuititia kwa mfumo wa utume. Kwa yakini, ni Khilafah pekee ndio itakayoweza kuunganisha wanajeshi wa Kiislamu kuweza kulinda Waislamu wa Filastin na biladi zote za Kiislamu.

Shabani Mwalimu
Mwakilishi kwa Vyombo vyatuhusu